TANGAZO LA SERIKALI NA. 515 la tarehe 21/6/2024

SHERIA YA FEDHA ZA SERIKALI ZA MITAA,
(SURA YA 290)

# SHERIA NDOGO

*(Imetengenezwa chini ya kifungu cha 16(1))*

SHERIA NDOGO YA HIFADHI YA BARABARA NA USHURU WA MAEGESHO YA HALMASHAURI YA JIJI LA ARUSHA YA MWAKA 2024

Jina

1. Sheria Ndogo hii itajulikana kama Sheria Ndogo ya Hifadhi ya Barabara na Ushuru wa Maegesho ya Halmashauri ya Jiji la Arusha ya Mwaka 2024.

Matumizi

2. Sheria Ndogo hii itatumika katika eneo lote la Halmshauri ya Jiji la Arusha.

Tafsiri

3 Katika Sheria Ndogo hii, isipokuwa kama muktadha utahitaji vinginevyo;

"Afisa Mwidhiniwa" maana yake ni afisa yeyote aliyeteuliwa na Mkurugenzi kwa lengo la kusimamia utekelezaji wa Sheria Ndogo hii;

"chombo cha usafiri" maana yake ni chombo chochote kinachotumika kusafirishia bidhaa, abiria au mizigo;

"basi kubwa" maana yake ni chombo cha usafiri cha kusafirisha abiria kuanzia 50 au zaidi kwa mkupuo mmoja;

"basi la kati" maana yake ni chombo cha usafiri cha kusafirishia abiria kuanzia kuanzia 19 hadi 49;

"basi dogo" maana yake ni chombo cha usafiri cha kusafirishia abiria kuanzia 5 hadi 18;

"Halmashauri" maana yake ni Halmashauri ya Jiji la

Arusha;

"kibali" maana yake ni idhini au ruhusa ya maandishi inayotolewa na Halmashauri;

"gari binafsi" maana yake ni gari lolote la mtu au kampuni binafsi ambalo halifanyi biashara;

"kituo cha mabasi" maana yake ni eneo maalumu lililotengwa au kujengwa na Halmashauri kwa ajili ya kupakia na kushusha abiria au mizigo;

"kituo cha teksi" maana yake ni kituo kilichosajiliwa na Halmashauri kwa ajili ya kuegesha teksi;

"magari ya mizigo" maana yake ni gari lolote lenye uzito wa tani moja au zaidi lililosajiliwa kufanya shughuli za biashara kwenye mamlaka ya Halmashauri;

"maegesho" maana yake ni maeneo yaliyotengwa kwa ajili ya kuegesha magari au kulaza magari na inajumuisha stendi za mabasi;

"Mkurugenzi" maana yake ni Mkurugenzi wa Halmashauri ya Jiji la Arusha au afisa yeyote aliyeteuliwa kutekeleza majukumu ya Mkurugenzi;

"mmiliki" maana yake ni mmiliki, kondakta au dereva anayetumia chombo cha usafiri;

"teksi" maana yake ni gari yoyote iliyosajiliwa kwa ajili ya biashara ya kusafirisha abiria au watu yenye uwezo wa kubeba abiria wasiozidi wanne;

"ushuru" maana yake ni kiwango cha fedha kilichopangwa na Halmashauri kinachopaswa kulipwa na mmiliki wa gari linapoingia au kuegeshwa kituoni; na

"Wakala" maana yake ni mtu binafsi au kikundi cha watu, shirika, taasisi au kampuni ambayo imeteuliwa na Halmashauri kufanya kazi yoyote chini ya Sheria Ndogo hii kwa niaba ya Halmashauri.

Maegesho

4.-(1) Mtu hataegesha chombo cha usafiri nje ya eneo lililotengwa kwa mujibu wa Sheria Ndogo hii.

(2) Halmashauri, kwa kushirikiana na taasisi nyingine, itaweka alama za barabarani za kuonesha sehemu iliyotengwa kwa ajili ya kuegesha vyombo vya usafiri.

(3) Halmashauri itaanzisha na kuainisha maeneo maalumu yatakayotumika kwa ajili ya kuegesha vyombo vya usafiri.

(4) Halmashauri inaweza kuchora mistari kwenye hifadhi ya barabara za mitaa ili kuonesha sehemu ambazo vyombo vya usafiri vinatakiwa kuegeshwa.

Mamlaka ya kutoza ushuru

5. Halmashauri itakuwa na mamlaka ya kutoza ushuru wa maegesho kwa mtu, taasisi au kampuni kwa ajili ya maegesho ya chombo cha usafiri.

Ushuru

6.-(1) Mtu yeyote anayehusika na chombo cha usafiri, isipokuwa teksi na magari binafsi ya kukodi, atawajibika kulipa ushuru wa maegesho wa eneo husika la maegesho.

(2) Halmashauri itatoza ushuru katika eneo lote la Halmashauri kwa mtu yeyote aliyeegesha chombo cha usafiri binafsi au biashara katika eneo la umma.

(3) Halmashauri itatoza ushuru magari yote yatakayoegeshwa kwenye eneo la hifadhi ya barabara.

(4) Ushuru wa maegesho utatozwa kwa viwango vilivyoainishwa katika Jedwali la Kwanza.

Vituo vya mabasi

7.-(1) Halmashauri itaanzisha vituo vya mabasi mahsusi kwa ajili ya kupakia na kushusha abiria na mizigo.

(2) Bila kuathiri kanuni ndogo ya (1), kampuni, taasisi au mtu binafsi anaweza kuanzisha na kusimamia kituo cha mabasi anayomiliki kwa nia ya kupakia na kushusha abiria na mizigo kwa kibali maalumu kutoka kwa Halmashauri.

(3) Mmiliki au dereva wa chombo cha usafiri kinachosafirisha abiria ndani na nje ya Halmashauri atapaswa kuingiza chombo hicho stendi ya Halmashauri na kulipa ushuru isipokuwa kwa mmiliki au dereva wa chombo cha usafiri aliyepata kibali chini ya kanuni ndogo ya 15(2) ambaye atalipia ushuru wa stendi kwa Afisa Mwidhiniwa.

(4) Kituo cha mabasi cha Halmashauri kinaweza

kutumika kwa ajili ya kuegesha na kulaza vyombo vya usafiri.

Ushuru wa vituo vya mabasi

8.-(1) Halmashauri itatoza ushuru wa stendi kwa vyombo vya usafiri vinavyoingia na kutoka ndani ya stendi kwa saa ishirini na nne.

(2) Baada ya kulipa ushuru wa stendi, dereva wa chombo cha usafiri atapewa stakabadhi ya kielektroniki inayolingana na malipo yaliyofanyika.

Kuanzishwa kwa maeneo ya kuegesha pikipiki

9.-(1) Halmashauri itatenga maeneo maalumu kwa ajili ya kuegesha pikipiki kadri itakavyoona inafaa.

(2) Dereva wa pikipiki atawajibika kuegesha pikipiki yake katika eneo lililotengwa kwa ajili hiyo.

(3) Halmashauri itatoza ushuru kwa kila pikipiki itakayoegeshwa katika eneo la maegesho ya pikipiki kama ulivyoainishwa katika Sheria Ndogo hii.

Kuzingatia utaratibu wa maegesho

10. Kila dereva wa pikipiki atatakiwa kuzingatia utaratibu uliowekwa na Halmashauri katika maeneo yaliyotengwa kwa ajili ya maegesho ya pikipiki.

Kuanzishwa kwa vituo vya magari ya mizigo

11.-(1) Halmashauri itaanzisha vituo maalumu kwa ajili ya kupakia na kushusha mizigo na kuegesha magari ya mizigo.

(2) Vituo vya magari ya mizigo vitaanzishwa na kusimamiwa na Halmashauri, isipokuwa kwamba Halmashauri inaweza kutoa kibali maalumu kwa mtu binafsi kuanzisha na kusimamia kituo na kitatumika kwa ajili ya magari ya mizigo tu.

Usajili wa magari ya mizigo

12. Kila mmiliki wa gari la mizigo linalofanya shughuli zake ndani ya Halmashauri atahakikisha gari lake linasajiliwa na Halmashauri.

Wajibu wa kuingiza gari

13. Kila mmiliki wa gari la mizigo atakuwa na wajibu wa kuhakikisha kuwa gari lake linaingia kituo cha

la mizigo kituoni

magari ya mizigo au linaegeshwa sehemu maalumu iliyotengwa kwa ajili hiyo.

Ushuru wa magari ya mizigo

14.-(1) Halmashauri itatoza ushuru wa maegesho kwa kila gari la mizigo litakaloegeshwa kwenye maegesho ya magari ya mizigo.

(2) Ushuru wa maegesho ya magari ya mizigo utatozwa kwa viwango vilivyoainishwa katika Sheria Ndogo hii.

Kituo na maegesho maalumu

15.-(1) Mtu au taasisi inaweza kuomba kituo au maegesho maalumu ya chombo cha usafiri kwa kujaza fomu ya maombi ya kituo au maegesho maalumu kama ilivyoainishwa katika Jedwali la Pili la Sheria Ndogo hii.

(2) Halmashauri itatoa kibali cha kituo au maegesho maalumu kwa mtu au taasisi iliyokubaliwa maombi kama kilivyoainishwa katika Jedwali la Tatu la Sheria Ndogo hii.

(3) Kibali cha kituo au maegesho maalumu kitakachotolewa chini ya kanuni ndogo ya (2) kitaainisha masharti ya matumizi ya kituo au maegesho maalumu na muda wa kibali.

Kufutwa kwa kibali cha Kituo na maegesho maalum

16.-(1) Halmashauri inaweza kufuta kibali cha kituo au maegesho maalumu endapo litajitokeza suala lolote kati ya yafuatayo:

(a) kuwepo kwa haja ya kutumia eneo husika kwa ajili ya ukarabati, uendelezaji, uboreshaji, upanuzi au shughuli yoyote inayohusu usimamizi wa barabara;

(b) kibali kimetolewa kwa mtu au taasisi kutumia eneo husika kwa ajili ya usimikaji wa miundombinu muhimu kwa huduma za jamii;

(c) kuna ukiukwaji wa masharti ya kibali; au

(d) kuendelea kuwepo kwa kituo au maegesho maalumu kunaonekana kutokuwa na tija au kuwa kinyume na maslahi ya umma.

(2) Endapo Halmashauri inakusudia kufuta kibali

cha kituo au maegesho maalumu, itatoa notisi ya maandishi ya siku thelathini kwa mtu aliyepewa kibali.

(3) Endapo kibali kitafutwa kwa sababu yoyote iliyoainishwa katika aya (a), (b) au (d) ya kanuni ndogo ya (1), Halmashauri itakuwa na wajibu wa kurejesha ushuru uliolipwa kwa muda uliosalia wa kibali.

Wajibu wa kulipa ushuru na kudai risiti

17.-(1) Kila mmiliki wa chombo cha usafiri atawajibika kulipa ushuru kama inavyoelekezwa katika Sheria Ndogo hii.

(2) Malipo ya ushuru wa maegesho yatafanyika kwa njia ya mfumo.

(3) Bila kuathiri masharti ya kanuni ndogo ya (1), mmiliki atakayelipa ushuru chini ya Sheria Ndogo hii atawajibika kudai risiti.

Mamlaka ya Halmashauri kwenye vyombo vya usafiri

18.-(1) Bila kuathiri masharti ya Sheria Ndogo hii, katika kusimamia maeneo ya maegesho, Halmashauri itakuwa na mamlaka ya-

(a) kuzuia kuondolewa kwa chombo cha usafiri kktoka katika eneo la maegesho;
(b) kukifunga chombo cha usafiri katika eneo la maegesho kwa kutumia kifaa maalum;
(c) kukinyanyua au kukivuta chombo cha usafiri kutoka katika eneo la maegesho kwa madhumuni ya kukihifadhi;
(d) kuondoa kitu chochote kinachohamishika kilichopo katika eneo la maegesho baada ya kutoa notisi ya siku saba kwa mmiliki wa kitu hicho; na
(e) kuuza kwa njia ya mnada, baada ya kupata amri ya Mahakama, kitu chochote ambacho kipo chini ya hifadhi ya Halmashauri kutokana na utekelezaji wa Sheria Ndogo hii kwa muda usiopungua miezi sita.

(2) Mtu yeyote hataruhusiwa kuchukua kitu chochote kilicho chini ya hifadhi ya Halmashauri kwa mujibu wa Sheria Ndogo hii isipokuwa tu kama mtu huyo

atakuwa amelipa gharama zote zilizoingiwa na Halmashauri katika kukiondoa na kukihifadhi kitu hicho kwa mujibu wa kanuni ndogo ya (1).

Zuio la kuegesha

19.-Halmashauri inaweza kuzuia kuegesha gari au chombo chochote cha usafiri katika eneo fulani kwa kuweka alama au kibao kilichoandikwa "Hakuna kuegesha hapa" au "No Parking" kwa sababu zifuatazo:

(a) kuongeza usalama kwa kurahisisha mzunguko wa magari;
(b) kuwepo kwa ujenzi au ubomoaji katika eneo husika; au
(c) sababu nyingine yoyote ambayo Halmashauri itaona inafaa.

Kuegesha kwa dharura

20.-(1) Halmashauri au Wakala anaweza kusamehe malipo ya ushuru kwa mtu yeyote atakayeegesha chombo cha usafiri kwa dharura.

(2) Bila kuathiri kanuni ndogo ya (1) mtu yeyote atakayeegesha chombo cha usafiri kwa dharura atatakiwa kuweka au kuonesha viashiria vya kuegesha chombo cha usafiri wakati wa dharura.

Vitendo visivyoruhusiwa

21. Vitendo vifuatavyo havitaruhusiwa kwa mmiliki wa chombo cha usafiri:

(a) kutengeneza au kuosha chombo cha usafiri ndani ya stendi;
(b) kuosha chombo cha usafiri katika maeneo yasiyoruhusiwa na Halmashauri;
(c) kuruhusu gari kuendelea kuwepo kituoni kwa zaidi ya masaa mawili;
(d) kuegesha au kulaza chombo cha usafiri kwenye maeneo ya barabara ambayo hayaruhusiwi;
(e) kuegesha chombo cha usafiri katika njia au katika eneo lolote lililotengwa maalumu kwa ajili ya waenda kwa miguu na barabara za huduma; au
(f) kuegesha gari kubwa la mizigo katika eneo tofauti

na maeneo yaliyoidhinishwa kwa mujibu wa Sheria Ndogo hii.

Msamaha wa ushuru wa maegesho

22.-(1) Vyombo vya usafiri vifuatavyo havitatakiwa kulipa ushuru wa maegesho:

(a) chombo cha usafiri kinachomilikiwa na Serikali chenye namba za usajili rasmi zinazotumiwa na vyombo vya usafiri vya Serikali;
(b) chombo cha usafiri kinachomilikiwa na taasisi yenye hadhi ya kidiplomasia chenye namba rasmi za usajili zinazotumiwa na vyombo vya usafiri vinavyomilikiwa na taasisi za kidiplomasia;
(c) chombo cha usafiri kinachoegeshwa katika maegesho yaliyo jirani na nyumba za ibada wakati wa ibada;
(d) chombo cha usafiri kinachoegeshwa katika maegesho yaliyo karibu na eneo linalotumika kwa muda huo kwa shughuli za kitaifa;
(e) chombo cha usafiri kinachotumiwa na mtu mwenye ulemavu kwa madhumuni yasiyo ya kibiashara; na
(f) chombo cha usafiri kwa ajili ya usafirishaji wa wagonjwa.

(2) Bila kuathiri masharti ya kanuni ndogo ya (1), Halmashauri inaweza, kwa kibali maalumu, kumruhusu mtu yeyote kutumia maegesho bila kulipa ushuru wa maegesho.

Muda wa utozaji wa ushuru wa maegesho

23.-(1) Ushuru wa maegesho utatozwa kila siku kuanzia saa kumi na mbili kamili asubuhi hadi saa kumi na mbili kamili jioni.

(2) Ushuru wa maegesho utatozwa kwenye chombo cha usafiri endapo kitaegeshwa kwa zaidi ya dakika tano katika eneo la maegesho.

(3) Bila kuathiri masharti ya kanuni ndogo ya (1) na (2), ushuru wa maegesho utatozwa kwa saa, siku, wiki, mwezi au mwaka.

Uteuzi wa Wakala

24.-(1) Halmashauri inaweza kuteua Wakala ili kukusanya ushuru wa maegesho kwa niaba yake chini ya Sheria Ndogo hii.

(2) Wakala aliyeteuliwa kwa mujibu wa kanuni hii atakuwa na wajibu wa-

(a) kukusanya na kupokea ushuru wa maegesho kwa kutumia mfumo wa kielektroniki kwa niaba ya Halmashauri katika eneo alilopangiwa na kwa viwango vilivyoidhinishwa katika Sheria Ndogo hii;
(b) kusimamia eneo la maegesho na kuchukua, kwa njia ya kielektroniki au njia nyingine itakayoidhinishwa na Halmashauri, kumbukumbu zote za vyombo vya usafiri vinavyoegeshwa katika eneo la maegesho na kuziwasilisha kwa Halmashauri; na
(c) kuwasilisha makusanyo yote kwa kuzingatia masharti ya mkataba wa uwakala alioingia na Halmashauri

Makosa

25. Mtu anatenda kosa ikiwa-

(a) anakataa au anakwepa kulipa ushuru;
(b) anaosha gari au anafanya matengenezo ya gari ndani ya eneo la stendi;
(c) anapakia abiria au mizigo katika sehemu isiyoruhusiwa;
(d) anamzuia kwa njia yoyote ile Afisa Mwidhiniwa au wakala kukusanya ushuru;
(e) anamshawishi mtu au kundi la watu kukataa kulipa ushuru;
(f) analaza gari katika barabara za Halmashauri;
(g) anaegesha gari katika eneo ambalo haliruhusiwi kwa ajili ya maegesho;
(h) anaanzisha au anaendesha kituo cha mbasi au maegesho bila kibali cha Halmashauri;
(i) anaharibu miundombinu ya maegesho; au
(j) anaegesha gari vibaya katika eneo la maegesho.

Adhabu

26.-(1) Mtu atakayetiwa hatiani kwa kosa lolote chini ya Sheria Ndogo hii atawajibika kulipa faini ya kiasi kisichopungua shilingi laki mbili na kisichozidi shilingi milioni moja au kifungo kisichopungua miezi kumi na mbili na kisichozidi miezi ishirini na nne au adhabu zote.

(2) Pamoja na adhabu katika kanuni ndogo ya (1), mtu atakayekutwa na hatia kwa kosa la kuharibu miundombinu ya maegesho atakuwa na wajibu wa kurekebisha miundombinu hiyo kwa madhumuni ya kuirejesha katika hali yake ya awali chini ya usimamizi wa Halmashauri au kulipa kwa Halmashauri gharama za marekebisho husika.

Kufifilisha kosa

27. Mkurugenzi atakuwa na uwezo wa kufifilisha kosa kwa kumtoza mtu yeyote aliyetenda kosa kinyume cha Sheria Ndogo hii kiasi cha shilingi laki mbili endapo mkosaji atakiri kosa na kuwa tayari kujaza fomu maalum iliyoainishwa katika Jedwali la Nne la Sheria Ndogo hii na kulipa ada au ushuru anaodaiwa.

______________

JEDWALI LA KWANZA

____________

*(Limetengenezwa chini ya aya ya 6(4))*

SEHEMU A:

USHURU WA MAEGESHO YA MAGARI BINAFSI NA YA BIASHARA

| Na. | Aina ya Chombo cha Usafiri | Muda wa kuegesha | Kiwango cha ushuru (Shilingi) |
|---|---|---|---|
| 1 | Gari binafsi la kutembelea | Kuanzia dakika 5 hadi saa 1 | 500/= |
| | | Siku nzima | 1,500/= |
| 2 | Gari kubwa la mizigo tani 3.5-tani 7 | Kuanzia dakika 5 hadi saa 1 | 1,000/= |
| | | Siku nzima | 3,000/= |
| 3 | Gari kubwa la mizigo kuaniza tani 7na kuendeea | Kuanzia dakika 5 hadi saa 1 | 1,500/= |
| | | Siku nzima | 5,000/= |
| 3 | Pickup au gari nyingine ndogo za mizigo | Kuanzia dakika 5 hadi saa 1 | 500/= |
| | | Siku nzima | 2,000/= |

SEHEMU B:

USHURU WA VITUO VYA MABASI (STENDI)

| Na. | Aina ya Chombo cha Usafiri | Kiwango cha Ushuru (Shilingi) | MUDA |
|---|---|---|---|
| 1 | Basi kubwa | 5,000/= | Kila linapotoka |
| 2 | Basi la kati (Costa) | 2,000/= | Kila linapotoka |
| 3 | Basi dogo | 1,000/= | Kila linapotoka |
| 4 | Gari binafsi inayoingia na kutoka stendi | 500/= | Kila linapotoka |
| 5 | Pikipiki za magurudumu matatu | 500/= | Kila linapotoka |
| 6 | Teksi zinazoingia | 500/= | Kila linapotoka |

*Tangazo la Serikali Na. 515 (Linaendelea)*

| | | | |
|---|---|---|---|
| | stendi | | |
| 7 | Mtu binafsi anapoingia stendi | 200/= | Kila linapotoka |
| 8 | Baiskeli inapoingia stendi | 200/= | Kila linapotoka |
| 9 | Mkokoteni | 500/= | Kila unapotoka stendi |
| 10 | Gari lolote linapolazwa stendi kuu | 5,000/= | Kwa usiku mmoja |
| 10 | Hiace zinazolala stendi za usafiri wa ndani ya Halmashauri | 2,000/= | Kila usiku mmoja |
| 13 | Pikipiki ikilala stendi za usafiri wa ndani ya Halmashauri | 1,000/= | Kila usiku mmoja |
| 14 | Bajaji au guta likilala stendi za usafiri wa ndani ya Jiji | 1,000/= | Kila usiku mmoja |

SEHEMU C:
USHURU WA MAEGESHO YA PIKIPIKI ZA MAGURUDUMU MAWILI NA MATATU

| Na. | AINA YA PIKIPIKI | Kiwango cha Ushuru (Shilingi) | MUDA |
|---|---|---|---|
| 1 | Pikipiki za magurudumu mawili | 300/= | Kwa siku |
| 2 | Pikipiki za magurudumu matatu | 500/= | Kwa siku |

SEHEMU D
ADA YA KIBALI CHA KUANZISHA KITUO CHA MABASI AU MAEGESHO MAALUMU

| Na. | Aina ya Kituo au Maegesho | Kiwango cha ada | MUDA |
|---|---|---|---|
| 1. | Kituo cha mabasi | 300,000/= | Kwa Mwaka |
| 2. | Magari makubwa | 100,000/= | Kwa mwaka |
| 3. | Magari madogo | 50,000/= | Kwa mwaka |

JEDWALI LA PILI

*(Limetengenezwa chini ya kanuni ya 15(1))*

MAOMBI YA KIBALI CHA KITUO AU MAEGESHO MAALUMU

Fomu Na……........….

*Tangazo la Serikali Na. 515 (Linaendelea)*

Jina la Mwombaji:..………....…………………..……………….....
Anwani ya Mwombaji:……………………..…..………..........
Namba ya simu ya Mwombaji:...................................................
Mahali anapoishi:.......................................................................
Ukubwa wa eneo la Kituo au maegesho linaloombewa kibali (meta za mraba):…...…..
Eneo analoomba kwa ajili ya Kituo au maegesho: Mtaa:.……barabara:.......Jengo:.......
Maelezo mengine (ikiwa yapo).......................................................................
Ninakiri kusoma, kuyaelewa na kukubali masharti ya kibali cha Kituo au maegesho maalumu.

Jina:………………………………………………………..........…………

Wadhifa:……………………………………………......…………………

Saini:……………………………………………........………………………
Tarehe:.……………………………………….......…………………………

---

JEDWALI LA TATU

*(Limetengenezwa chini ya kanuni ya 15(2))*

KIBALI CHA KITUO AU MAEGESHO MAALUM

Kibali Na....................

Jina: ....................................................................................................
Anwani: ...........................................................................................
Namba ya Kitambulisho cha Taifa: .........................SIMU.........................
Namba ya Stakabadhi: .....................amelipa Sh.....................................
Eneo lilipo: Mtaa:..……………barabara:……..Jengo:…………......…
Ukubwa wa eneo la Kituo au Maegesho (mita za mraba):………......
Kiasi kilicholipwa kwa miezi Jumla ya sh.........................................
Muda wa kibali ni mwaka mmoja kuanzia..................hadi..................
Maelezo mengine yatakayohitajika (kama yapo):……………......….
Kimetolewa tarehe…………mwezi……………….mwaka………........…..

Kimetolewa na:-
Jina:……………………………………………………..……………..
Wadhifa:…………………………………………………….………………….
Saini................................................. Muhuri wa Ofisi:.…………....................

JEDWALI LA NNE

*(Limetengenezwa chini ya kanuni ya 27)*

HATI YA KUFIFILISHA KOSA

Mimi .........................................................................nakiri KWA HIARI YANGU MIMI MWENYEWE mbele ya........................................................... ambaye ni Mkurugenzi wa Halmashauri ya Jiji la Arusha kwamba Tarehe ..........ya Mwezi .................. Mwaka................ nilitenda kosa kwa kukiuka masharti ya kanuni ya ……..ya Sheria Ndogo ya Hifadhi ya Barabara na Ushuru wa Maegesho ya Halmashauri ya Jiji la Arusha ya Mwaka 2024.

Kwa Mamlaka aliyopewa Mkurugenzi wa Halmashauri niko tayari kulipa kiasi cha shilingi……………………………………………………………………. badala ya kushtakiwa Mahakamani.

NATHIBITISHA KWAMBA MAELEZO HAPO JUU NI YA KWELI NA NIMEYATOA MIMI MWENYEWE KWA HIARI YANGU KADRI YA UFAHAMU WANGU.

Leo Tarehe ......................ya Mwezi ................................Mwaka ………..…
Jina: .......................................................
Saini: .......................................................
MBELE YA:
Jina…….................................................
Wadhifa: ..................................................
Saini: .......................................................
Tarehe: ....................................................

Lakiri ya Halmashauri ya Jiji la Arusha imegongwa kwenye sheria ndogo hii kufuatia Azimio lililopitishwa katika Mkutano wa Baraza la Madiwani la Halmashauri Jiji la Arusha uliofanyika tarehe 03 Mwezi Novemba, 2023 na imegogwa mbele ya;

INJ. JUMA HAMSINI
Mkurugenzi wa Jiji la Arusha

MAXIMILIAN J. IRANQHE
*Meya wa Jiji la Arusha*

NAKUBALI,

L.S

Dodoma
20 Februari, 2024

MOHAMED OMARYMCHENGERWA
*Waziri wa Nchi ofisi ya Rais*
*(Tawala za mikoa na serikali za mitaa)*